**HOTUBA YA AFISA MTENDAJI MKUU WA MFUKO WA CHANGAMOTO ZA MILENIA NDUGU BERNARD MCHOMVU KWA MAKAMU WA RAISI ALIPOTEMBELEA MRADI WA UPANUZI WA MTAMBO WA KUCHUJIA MAJI WA RUVU CHINI TAREHE 14 MACHI 2013**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Kama unavyofahamu, Serikali ya Marekani kupitia MCC inagharamia miradi mbali mbali nchini. Kiserikali MCA-T imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi inayohusika ni kama ifuatavyo:-

Miradi ya Maji:

(i) Upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji hapa Ruvu chini kwa ajili ya Jiji la Dar es salaam na sehemu za Mkoa wa Pwani ikiwemo Wilaya ya Bagamoyo. Kazi muhimu inahusisha upanuzi wa mtambo mpya wa kuchujia maji pamoja na miundombinu mingine inayotakiwa;
(ii) Ukarabati wa mfumo wa maji kwa mji wa Morogoro unaohusisha ujenzi wa mtambo mpya wa maji eneo la Mambogo na ukarabati wa mtambo wa Mafiga. Kazi hii inajumuisha pia ujenzi wa bomba kuu kati ya Mafiga na Tumbaku pamoja na ukarabati na ujenzi wa matenki mapya; na
(iii) Mradi wa kupunguza maji yasiyolipiwa kwa jiji la Dar es salaam..

Miradi ya Barabara:

(i) Ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro;
(ii) Ujenzi wa barabara ya Tunduma – Sumbawanga;
(iii) Ujenzi wa barabara za Peramiho – Mbinga na Songea – Namtumbo;
(iv) Ujenzi wa barabara tano za vijijini katika kisiwa cha Pemba; na
(v) Uwekaji lami katika kiwanja cha ndege cha Mafia

Miradi ya Umeme:

(i) Mradi wa kupeleka umeme Zanzibar (katika kisiwa cha Unguja) kutoka katika gridi ya Taifa kupitia chini ya bahari;
(ii) Uimarishaji na upanuzi wa mtandao wa umeme katika mikoa saba ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma , Mwanza na Kigoma
(iii) Mradi wa umeme wa jua Mkoani Kigoma.

Miradi hii yote imekwishaanza na baadhi yake imekamilika na hii ni kama vile Tanga – Horohoro, usambasaji umeme Dodoma, mradi wa

kupeleka umeme Zanzibar ambao kwa sasa uko katika hatua za mwisho za kufanyiwa majaribio na mradi wa usambaji umeme Sengerema. Uwanja wa ndege wa Mafia utakamilika hivi karibuni iwapo mvua hazitakuwa nyingi.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

- Mradi wa Upanuzi wa mtambo wa kuchujia maji wa Ruvu chini ni sehemu ya utekelezaji wa oboreshaji wa huduma za maji kwa jiji la Dar es salaam na miji ya Bagamoyo Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Millenia (MCC).

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

- Kazi ya kusanifu na kuandaa zabuni ilianza Juni 2009 na ilikamilika mwaka 2010 na kazi ya kutafuta mkandarasi ilianza
- Mkataba wa Upanuzi wa Mtambo wa kusafishia maji wa Ruvu chini ulitiwa saini tarehe 27 Januari 2011 kati ya **Mtendaji Mkuu – Mfuko wa Maendeleo ya Milenia – Tanzania** kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muunganiko wa Kampuni ya **Degremont Spencon Consortium** kutoka nchini Ufaransa na Kenya. Ujenzi wa mradi huu utagharimu kiasi cha Dola za Marekani 36,880,012.38 Milioni.
- Mkataba wa usimamizi wa ujenzi wa mtambo ulitiwa saini kati ya **Mtendaji Mkuu – Mfuko wa Maendeleo ya Millenia – Tanzania** kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kampuni ya **UWP Consulting (PTY) ya Afrika Kusini** kwa gharama ya $2,678,000.00 na hivyo gharama za mradi mzima kuwa $ 39,558,012.38

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Upanuzi wa mtambo huu unahusisha maeneo yafuatayo:

- Ujenzi wa kituo kipya cha kusukumia maji ghafi kikiwa na pampu mpya; kituo hiki kimekamlika kwa asilimia 88 ambapo jengo limekamilika, pampu za kusukuma maji zimewasili na kazi ya kuzifunga imeanza

- Ujenzi wa sehemu mpya ya kugawanyisha maji (combined flow dividing/mixing unit). Ujenzi wa sehemu hii umekamilika kwa asilimia 92, kazi kubwa iliyobakia ni kupaka rangi na kufunga nyaya za umeme
- Ujenzi wa mtambo wa kuondoa taka kwenye maji (Clarifier)- Mtambo huu umekamilika kwa asilmia 88. Kazi zinazoendelea ni pamoja na uwekaji wa mabomba ya kusambaza na ugawaji wa maji kwenye mtambo (distribution pipes)
- Ujenzi wa chujio jipya la kusafishia maji umekamilika kwa asilimia 87% na kazi zinazoendelea ni pamoja na uwekaji wa miundombinu kwa ajili mchanga wa kuchuja maji pamoja na ujenzi wa tenki jipya la kuhifadhia maji yaliyosafishwa lenye uwezo wa kutunza mita za ujazo 24,000.Tenki hili limekamlika kwa asilimia 98,kazi zinazoendelea kulimalizia ni pamoja na kupaka rangi na kuweka mifuniko.

- Ujenzi wa kituo kipya cha kusukumia maji yaliyosafishwa; Kituo hiki kimekamlika kwa asilimia 58, kazi zinazoendelea ni kukamilisha jengo, pampu za kusukuma maji zimewasili na kazi ya kuzifunga itanza mwezi ujao.

  Ujenzi wa bwawa la kusafishia maji taka (sludge lagoon); Bwawa hili limekamilika kwa asilimia 98, kazi iliyobaki ni kuunga mabomba na kupanda nyasi pembeni

- Kazi nyinginezo muhimu ziendanazo na mtambo huu na hasa mabomba, uboreshaji wa mfumo wa umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo, barabara, uzio n.k. ziko katika maandalizi ya kuanza ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mabomba ambao umekamilika, kuagiza vifaa vya umeme na mitambo. Kazi zingine kama ujenzi wa mifumo ya barabara na uzio zitafanyika mwishoni baada ya kumaliza ujenzi wote.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

- Utekelezaji wa mradi ni wa kuridhisha ukiwa umefikia kiwango cha jumla cha asilimia 81. Kimkataba mradi ulitegemewa ukamilike mwezi Machi 2013 lakini kutokana na sabababu mbalimbali kwa sasa mradi unategemewa ukamilike ifikapo mwezi Julai 2013. Baada ya hapo

usukumaji wa maji utategemea tu kukamilika kwa bomba jipya linalojengwa sasa hivi.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

- Kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu chini kutaongeza uzaliashaji wa maji toka kiwango cha sasa cha lita za ujazo 180 milioni hadi lita za ujazo 270 milioni kwa siku na hivyo kuboresha huduma za upatikanaji wa maji ambayo kwa muda mrefu imekuwa ni kero kubwa kwetu sote tunaoishi Dar es salaam na maeneo ya Bagamoyo, Bunju, Boko, Tageta, Mbezi beach, Mikocheni, Mwenge, Sinza na katikati ya Jiji. Kukamilika kwa mradi huu pia kutachangia kuboresha afya za wakazi wa Dar es Salaam na utakuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa Taifa hasa ikizingatiwa kuwa Dar es Salaam ni Jiji la viwanda na maji ikiwa ni nyenzo muhimu katika uzalishaji viwandani.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

- Katika kutekeleza mradi kama ilivyo kawaida ya miradi yote , tunakumbana na changamoto mbalimbali. Kubwa ikiwa ni uwezo na uchakavu wa bomba la sasa la kusafirishia maji kutoka Ruvu hadi Dar es salaam. Bomba hili lenye kipenyo cha mita 1.350 lilijengwa miaka ya mwanzoni mwa sabini. Tunafarijika kwamba bomba jipya limeanza kujengwa na litakamilika mwaka huu au mapema mwakani.

**MHESHIMIWA MAKAMU WA RAIS NAOMBA KUWASILISHA NA KARIBU UTEMBELEE MRADI**